

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**



**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**MKUTANO WA TATU**

**KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI**

**20 MEI, 2021**



## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

### MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA MBILI – TAREHE 20 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:**

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha

2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**III. MASWALI:**

**WIZARA YA MADINI:**

**272. MHESHIMIWA GHATI ZEPHANIA  
CHOMETE (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa  
Madini:-

Je, Serikali ina Teknolojia gani mbadala ambayo itaepusha kutumia magogo kama matimba kwenye mashimo ya migodi hasa maeneo ya Nyamongo, Tarime, Buhemba na Butiama.

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,  
JINSIA, WAZEE NA WATOTO:**

**273. MHESHIMIWA ZAYTUN SEIF SWAI (VITI  
MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mkakati gani dhidi ya vitendo vya ukatili vinavyofanywa kwa Wanawake na Watoto.

**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:**

**274. MHESHIMIWA VINCENT PAUL MBOGO (NKASI KUSINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, ni lini Serikali itatatua mgogoro kati ya Hifadhi ya Lwafi iliyopo Nkasi Kusini na Wananchi wa Vijiji vya Mlambo, King'ombe, Tundu na Kata ya Wampembe.

**WIZARA YA MAJI:**

**275. MHESHIMIWA KASSIM IDDI IDDI (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itanza kusambaza maji kutoka Mradi wa Maji Mhangu – Ilogi katika Kata za Lunguya, Ikinda, Shilela, Sogese na Mega katika Halmashauri ya Msalala.

**276. MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA (MBARALI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji Ruduga – Mawindi ili kuwatua ndoo kichwani Akina Mama wa Mbarali.

**IV. HOJA ZA SERIKALI:**

**WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA  
20 MEI, 2021**

**N. J. MWIHAMBI, *ndc*  
KATIBU WA BUNGE**